



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

Tangazo la nafasi ya kazi Meneja HSE – EACOP EITS Contractor MAREJEJO: 1046-ADVT-GAC EI-TZ-GEN-Meneja HSE

Schneider Electric Projects and Services Tanzania Limited (CONTRACTOR) kama Mkandarasi Mkuu wa EITS (Electrical Instrumentation and Telecommunications Systems) katika mradi wa EACOP, inahitaji huduma za Meneja HSE

Maelezo mafupi ya kazi:

Mwombaji atakuwa na jukumu la kuunga mkono shirika la ndani wa nchi la mkandarasi wa EITS Integrator na timu za utekelezaji wa mradi.

Kuendesha ajenda ya Afya, Usalama na Mazingira kwa Mkandarasi Mshirikishi wa EITS katika maeneo na ofisi zenye msingi wa kusaidia shughuli za mradi zilizo kando ya bomba.

Majukumu makuu:

- Kuhakikisha utambuzi, ufuatiliaji na mapitio ya sheria na kanuni za HSE
- Kuhakikisha ukaguzi wa uzingatiji wa sheria za OSHA unafanywa angalau mara moja kwa mwaka kulingana na sheria husika.
- Kuhakikisha, kwa kushirikiana na Idara ya Sheria, kwamba usimamizi wote wa sheria unaohusiana na HSE unafuata.
- Kushauri kuhusu mabadiliko ya sheria ya Afya, Usalama na Mazingira kadri yanavyoweza kuathiri utekelezaji wa mradi
- Kuendesha utekelezaji wa mchakato wa Tathmini ya Hatari ndani ya shirika
- Kufanya ukaguzi na tathmini inayohusu masuala ya HSE
- Kuendeleza mchakato na zana thabiti za usalama kulingana na taratibu za shirika: tathmini za hatari, ripoti, uchambuzi wa chanzo cha matukio, majadiliano ya kiufundi n.k.
- Kama inavyotumika kushirikisha EACOP Co. kuhusu kampeni na matangazo ya OHS kadri yanavyoweza kuwa muhimu kwa Mkandarasi Mshiriki wa EITS.
- Kuandaa miundo na ratiba za kuripoti kulingana na EACOP Co. na mahitaji ya mradi
- Kuandaa ratiba za mawasiliano
- Kuendesha mpango wa Uhamasishaji na kujikinga na

Malaria kwenye mradi

- Kusimamia uhusiano na mamlaka za ndani kuhusiana na HSE
- Kusaidia na kuongoza taratibu za ushiriki wa wafanyakazi kulingana na taratibu za OHS.
- Kuwa kiunganishi kati ya kampuni na wasimamizi wakuu wa usalama wa wakandarasi wa mradi.
- Kuandaa sera za usalama, taratibu na mipango ya usalama
- Kufanya tathmini za hatari za kiusalama na uwezekano wa kuathirika kwa wafanyakazi walipo kwenye maeneo mbalimbali ya mradi.
- Kuwa kiunganishi cha huduma husika zinazohusu Afya, Usalama na Mazingira

Sifa za mwombaji:

- Awe na Shahada ya Kwanza (au zaidi) katika Kozi ya Sayansi au Uhandisi kutoka Chuo Kikuu Kinachotambuliwa na kudihisinishwa.
- Awe na leseni/ cheti kwa mujibi wa sheria za ndani
- Awe na angalau uzoefu wa miaka 5 wa kazi ya umeneja wa HSE katika kampuni inayotambulika.
- Uwezo wa kuzungumza vyema Kiswahili na kingereza
- Awe na leseni hai ya udereva
- Awe na uwezo wa kuandaika, kuchapa na kuwasiliana vyema
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hususani program za Microsoft: WORD, EXCEL, POWERPOINT nk
- Awe na msukumo na kiwango cha juu cha uadilifu wa kitaaluma na kibinafsi

Sifa za ziada:

Uzoefu wa uongozi katika mazingira ya mashirika ya kimataifa na yenye changamoto.

- Uzoefu a katika usimamizi wa usalama wa vifaa vya viwandani.
- Uzoefu katika Sekta ya Mafuta na Gesi ni faida ya nyongeza

Wenye nia ya kutuma maombi na ambao wanakidhi vigezo vinavyohitajika na walio na uwezo wanapaswa kutuma wasifu wao (CV) kwa Kiingereza kupitia barua pepe ya eacop.eits@se.com; kwa marejejo 1046-ADVT-GAC EI-TZ-GEN-Meneja wa HSE ifikapo tarehe **28 Februari, 2023, 5:00pm**. Saa za Afrika Mashariki.

Waombaji tu wanaokidhi vigezo vinavyohitajika na kufaulu mtihani wa kuingia ndiyo watapata fursa ya kujumuishwa katika mchakato wa usaili. Tafadhali kumbuka kuwa, ikiwa hutapigiwa simu zaidi ya wiki mbili baada ya tarehe ya mwisho, tambua kuwa ombi lako halijafanikiwa. KAMPUNI inahifadhi haki ya kutozingatia waombaji ambao hawajafikidhi vigezo vinavyohitajika